



Mwanza Kwanza

Linatolewa: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza



/Mwanzakwanza

Toleo Namba 1 / 2020



Uwekezaji

Miundobinu

Ujasiliamali

MATOKEO YA UCHAGUZI MKUU 2020

JPM nambari 'one' Mwanza

**Ubunge,
udiwani
vyote
CCM
Mwanza**

NA MWANDISHI WETU

Wagombea Ubunge wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mwanza wameibuka vinara katika Uchaguzi Mkuu wa wabunge mkoani hapa baada ya kujizolea kura za kutosha katika uchaguzi uliofanyika Jumatano wiki hii.

Mmoja wa wagombea hao ni Dkt Angelina Mabula ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya kazi ambaye alikuwa anagombea kwa mara ya pili katika jimbo la Ilemela. Dkt Mabula amepata kura 147,724 sawa na asilimia 83.91 ya kura zote zilizopigwa katika jimbo lake.

Wagombea wengine walioshinda katika kinyang'anyiro hicho ni Mhe. Bonaventura Kiswaga wa Jimbo la Magu aliyepata kura 139,975 sawa na asilimia 88.93 ya kura zote zilizopigwa, Mhe. Joseph Mkundi wa Jimbo la Ukerewe aliyepata kura 91,893 sawa na asilimia 78.74% na Mhe. Eric Shigongo wa Jimbo la Buchosa aliyepata kura 79,950 sawa na asilimia 86.44.

Wengine ni Mhe. Slanslaus Mabula aliyepata kura 73,591 sawa na asilimia 61.80, Mhe. Tabasamu Mwaguuo aliyepata kura 59,734 sawa na asilimia 87.61, Mhe. Shanif Mansoor wa Jimbo la Kwimba aliyepata kura 57,943 sawa na asilimia 95.33 na Kasalali Mgeni wa Jimbo la Sumve aliyepata kura 31,373 sawa na asilimia 81.74.

Mgombea Ubunge wa Jimbo a Misungwi, **INAENDELEA UK 4**



Mwanza tupo shwari - RC Mongella **UKURASA 2** ▶



Ujumbe wa *Mkuu wa Mkoa*

John Mongella

Mwanza tupo shwari

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. John Mongella amesema kwamba kampeni za uchaguzi mkoani humu ziliendeshwa vizuri na kwa usalama, wagombea wote wakibea ajenda ya maendeleo ambayo kila mwananchi anayataka.

Akizungumza mara baada ya kupiga kura katika kituo cha kupiga kura cha Kiseke Polisi, Mhe. Mongella amewaomba wana Mwanza wote waendeleze kuwa watulivu kama wanavyojulikana.

"Niwaombe wana Mwanza wote kama ambavyo tunajulikana wakati wote kuwa na utulivu katika mkoaa wetu, tuendelee kuwa watulivu tufuate sheria tufuate taratibu zinazotuongoza. Ajenda ya mwaka huu kama wagombea wenye wote wame-sisitiza, hakuna aliyesisitiza vinginevyo ni kutaka maendeleo makubwa zaidi", alisema

Mongella

Mkoaa wa Mwanza unajumla ya wapiga kura 1,844,641 wilaya saba na Halmashauri nane huku jumla ya majimbo tisa ambayo yote kwa pamoja yanatengeneza jumla ya vituo yya kupigia kura 4996.

Majimbo hayo ni Nyamagana ambayo imeandikisha wapiga kura wengi zaidi (348,891) na Sumve ambayo inawapiga kura wachache zaidi (94,029). Majimbo mengine ni Kwimba, Misungwi, Sengerema, Ukerewe, Ilemela, Magu na Buchosa.

Wakati wa kampeni, viongozi mbalimbali wa dini wamekuwa wakitoa matamko mbalimbali wakisisitiza wagombea wa vyama mbalimbali na wafuasi wao na wananchi kwa jumla kuhakikisha kuwepo kwa amani na kutoshiriki katika vurugu.

Mmoja ya viongozi wa dini aliyetoka tamko

**Wakati wa kampeni,
viongozi mbalimbali
wa dini wamekuwa
wakitoa matamko
mbalimbali
wakisisitiza
wagombea wa
vyama mbalimbali
na wafuasi wao
na wananchi kwa
jumla kuhakikisha
kuwepo kwa amani
na kutoshiriki katika
vurugu.**

ni Askofu Dkt. Charles Sekelwa ambaye ni Mwenye kisha Mwenza wa Kamati ya Amani ya viongozi wa dini mkoani Mwanza aliitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutenda haki kwenye uchaguzi.

"Tume ya Taifa ya Uch-

agazi itende haki kwa vyama na wagombea wote. Ihakikishe vituo vyote yya kupiga kura vinafunguliwa mapema na huku vituo hivyo vikiwa na vifaa vyote vinavyohitajika bila kusahau mahitaji ya watu wenye uhitaji maalum", alisema Askofu Sekelwa.

Kamati hiyo pia imewaomba wagombea na wananchi wote kukubali matokeo kwani katika ushindani ni lazima apatikane mshindi na atakayeshindwa, na hii itaepusha vuru-gu zitakazo pelekea uvunjifu wa Amani.

"Amani ikitoweka itaathiri watu wote bila kujali aliyeianzisha, aliyehamasisha na atakayevunja kwani hakutakuwa na shughuli zozote kiuchumi zitakazoweza kufanyika, biashara hazitafanyika, shule, hospital haken-deki, usafiri hautokuwepo kwani vituo yya mafuta havitafanya kazi", Aliongeza.

Naye Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Sheikh Hassan Kabeke akizungumza katika mkutano huo amewataka wazazi wakae na vijana wao na kuwaeleza umuhimu wa amani na kujizuiakuingia katika mambo yoyote yanayoweza kuleta vurugu na kupelekea uvunjifu wa amani.



Gazeti hili linatolewa: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza
Regional Drive Mkabala na Ofisi za TRA
P.O. Box 119, Mwanza



+255 028 2501037



ras.mwanza@tamisemi.go.tz

Emmanuel Tutuba
Abel Ngapemba
Remija Salvatory
Barnabas Mkwayu



+255 028 2501037
0784 273 588
0783 317 188
0657 929 650



mwanza.go.tz

NA MWANDISHI WETU

Wananchi wa mkoa wa Mwanza wameonyesha imani kubwa kwa Mgombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM) katika Uchaguzi Mkuu, Mhe. John Pombe Magufuli kwa kumchagua kumpa jumla ya kura 944,463 kati ya kura halali 1,050,311 zilizopigwa Jumatano ili-yopita.

Kura hizo ni sawa na asilimia 89.92 ya kura zote halali za urais zilizopigwa katika majimbo tisa ya uchaguzi ya mkoa wa Mwanza yaliyokuwa na jumla la vituo 4,996 vya kupigia kura.

Majimbo hayo ni Ukerewe ili-yokua na vituo 522, Magu iliyokuwa na vituo 540, Kwimba iliyokuwa na vituo 310, Sumve iliyokuwa na vituo 265, na Misungwi iliyokuwa na vituo 549.

Majimbo mengine ni Sengerema iliyokuwa na vituo 557, Buchosa iliyokuwa na vituo 563, Ilemela iliyokuwa na vituo 795 na Nyamagana ambayo ilikuwa na jumla ya vituo 895.

Kulingana na daftari la wapiga kura, wananchi waliojiandikisha kupiga kura walikuwa 1,845,816, aki-ni walijitokeza kupira kura walikuwa 840,238. Katika idadi hiyo, kura 11,174 ziliharibika.

Aliyemuuta Rais Magufuli ni mgombea wa Chama cha Maendeleo na Demokrasia (CHADEMA) Mhe. Tundu Lissu ambaye alipata kura 95,409 sawa na asilimia 9.0 na kufuatiwa na mgombea wa CUF ali-yepata kura 1,216 sawa na asilimia 0.13 na ACT ali-yepata kura 1,151 sawa na asilimia 0.1.

Vyama vingine vilivyobaki (NCCR Mageuzi, Demokrasia Makini, ADC, NRA, UDP, AAFP, CHAUMMA, ADA TADEAM UPDP, SAU, TLP, UMD na DP) kwa ujumla wao vilipata kura 8,072 sawa na asilimia 0.89 sawa na



asilimia 0.78.

Mkoa wa Mwanza ni moja ya mikoa ambayo Mhe. Magufuli alipa-ta mapokezi makubwa mwezi Septemba wakati wa kampeni ambako maelfu ya wananchi walijitokeza katika mikutano yake, hasa mkubwa uliofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba na pia katika mikutano aliyokuwa akiifanya njiani baada ya kuzuiwa na wananchi wazungumze naye.

Katika mikutano yote ya kampeni hapa Mwanza, Rais Magufuli pia alikuwa akiwanadhi wagombea wa CCM

kwa nafasi ya ubunge na udiwani. Wagombea wa ubunge wote tisa wameshinda katika uchaguzi huo akiwemo aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi Dkt Angelina Mabula. Mbunge mmoja kutoka jimbo la Misungwi, Mhe. Alexander Mnyeti alipita bila kupingwa.

Katika kinyaganyilo cha nafasi ya udiwani CCM imeshinda katika kata 189 kati ya kata 191 zilizopo. Kata mbili zilizopo Jimbo la Sumve zimechukuliwa na madiwani wa CHADEMA.

JPM nambari ‘one’ Mwanza

Matokeo ya urais Kitaifa yaliyotangazwa na NEC

MGOMBEA	CHAMA	KURA	ASILIMIA
Magufuli John Joseph	CCM	12,516,252	84.40%
Tundu Antipas Lissu	Chadema	1,933,271	13.04%
Bernard Kamillius Membe	ACT Wazalendo	81,129	0.55%
Ibrahim Haruna Lipumba	CUF	72,885	0.49%
Hashim Spunda Rungwe	Chauma	32,878	0.22%
Seif Maalim Seif	AAFP	4,635	0.03%
John Paul Shibuda	ADA-Tadea	33,086	0.22%
Cecilia Augustino Mwanga	D.Makini	14,556	0.10%
Yeremia Kulwa Maganja	NCCR-Mageuzi	19,969	0.13%
Muttamwega Bhatt Mgaywa	SAU	14,922	0.10%
Twalib Ibrahim Kadege	UPDP	6,194	0.04%
Queen Cuthbert Sendiga	ADC	7,627	0.05%
Khalfan Mohammed Mazrui	UMD	3,721	0.03%
Philipo John Fumbo	DP	8,283	0.06%
Leopold Lucas Mahona	NRA	80,787	0.54%



Ubunge, udiwani vyote CCM Mwanza

INATOKA UK 1 Alexander Mnyeti alipita bila kupingwa na hivyo kufanya vitu vyote vya ubunge katika mkoa wa Mwanza vyote kwenda cha CCM.

Mbali na nafasi hizo za ubunge, CCM imezoea pia viti karibu vyote vya udiwani katika kata zote za mkoa huo isipokuwa kata mbili zilizopo katika Jimbo la Sumve ambazo zimechukuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Kata hizo ni za Nkalalo na Mwabomba.

Mkoa wa Mwanza unajumla ya kata 191 ambazo kati yake, CCM imechuka kata 189. Majimbo hayo ni Ukerewe yenye kata 25, Magu (25), Kwimba (15), Sumve (15) na Sengerema (26). Majimbo mengine ni Buchosa (21), Illemela (19) na Nyamagana (18).

Kulingana na daftari la wapiga kura, Mkoa wa Mwanza ulikuwa na wapiga kura 1,844,641 na kulikuwa na jumla ya vituo vya kupigia kura vifatavyo 4,996.



Bonaventura Kiswaga



Shanif Mansoor



Eric Shigongo



Alexander Mnyeti



Slanslaus Mabula



Dkt. Angelina Mabula



Wanawake, vijana Mwanza wakopeshwa Sh. bil 2.1

MWANDISHI WETU

Suala la uwezesaji kiuchumi ni kati ya mambo yanayopewa kipaumbibe na Serikali kwa nia ya kuwezesha Watanzania wengi kushiriki shughuli za uzalishaji na ujenzi wa uchumi wa Taifa.

Mikopo kwa makundi ya vijana, wanawake na walemaru kuitia asilimia 10 ya bajeti za halmashauri ni moja ya mikakati hiyo inayotekelezwa na Serikali.

Mkoa wa Mwanza ni kati ya mikoa nchini ambayo siyo tu inatekeleza mikakati ya kuwawezesha wananchi kuitia mikopo, bali pia kutenga maeneo maalum ya kibashara kwa makundi husika.

Katika taarifa ya mkoa wa utekelezaaji wa Ilani ya CCM, mkoa wa Mwanza umetenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za kibashara na uwekezaji katika kila halmashauri.

Maeneo hayo kiwilaya ni pamoja na Sungura katika halmashauri ya Ukerewe, Nguduluguu na Icheja kwa Halmashauri ya wilaya ya Ksimba na Nyegezi, Makorobi, Sinai- Mabatini, Kituo cha Mabasi cha Tanganyika na Temeke-Gerage Area kwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela umetenga maeneo ya biashara Kiloleli, Buswelu, Buzuruga, Kirumba na Pasiansi wakati kwa Magu maeneo yaliyotengwa ni Isandula, Ihala, Itumbili na Ilungu huku Sengerema ikitenga maeneo ya Bujora, Bukala na Isungang'olo na Misungwi imetenga maeneo ya Usagara, Idetemiya na Misungwi mjini.

Mikopo kwa vijana

Jumla ya vikundi 215 kutoka halmashauri za mkoa wa Mwanza vimenufaika kwakupokea mikopo yenye thamani ya Zaidi ya Sh695.1 milioni.

Vikundi hivyo na idadi kwenye mabano ni Jiji la Mwanza (88), Manispaa ya Ilemela (33), Ukerewe (4), Sengerema (11), Ksimba (17), Magu (8), Misungwi (4) na Buchosa vikundi 50.

Vikundi vya walemaru

Aidha, jumla ya Sh663.7 milioni zime-tolewa kama mikopo kwa vikundi 67 vya watu wenye ulemarv ambapo wilayani Misungwi vukundi vitatu vimenufaika, Buchosa 7, Ksimba 14, Magu 2, Sengerema 6, Ukerewe 3, Ilemela 5 na Jiji la Mwanza vikundi 27. Baadhi ya shughuli ziza kiuchumi zinazofanywa na vikundi ni ununuzi na uuzaaji nguo (mitumba), biashara ndogo ndogo, ufugaji wa kuku, kuuza samaki, uuzaaji wa dagaa, vioski na upandaji miti kwa ajili ya biashara na kilimo cha bustani za mbogamboga.

Katika kuhakikisha kwamba Halmashauri zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu, mkoa umetenga jumla ya Sh707.3 milioni kwa mikopo kwa vikundi 491.

Uwezesaji wanawake

Mkoa umeendelea kuwawezesha wanawake wanawake kiuchumi kwa kuapatita elimu ya ujasiriamali na biashara ili kuwawezesha kuongeza ajira, ujuzi wa kujiali, na fursa za kipato na kujikumu



ambapo jumla ya wanawake 1,161 kutoka halmashauri nane za mkoa wa Mwanza wamepata mikopo.

Idadi ya wanufaika kwa kila halmashauri ni Magu-152, Ilemela-285, Misungwi-94, Ukerewe-56, Sengerema-105, Ksimba-120 na jiji la Mwanza ili-yopesha wanawake 351.

Aidha vikundi hivyo vilifundishwa mada mbalimbali kwa nadharia na vitendo pamoja na namna ya kuanzisha biashara; kutunza mahesabu, uten-genezaji wa bidhaa kama sabuni za maji, batiki utafutaji wa masoko ya bidhaa hizo pamoja na vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya uwezesaji wanawake kiuchumi.

Katika kuhakikisha kwamba Halmashauri zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye

Jumla ya vikundi 215 kutoka halmashauri za mkoa wa Mwanza vimenufaika kwakupokea mikopo yenye thamani ya Zaidi ya Sh695.1 milioni

masharti nafuu, mkoa umetenga jumla ya Sh707.3 milioni kwa mikopo kwa vikundi 491.

Vikundi hivyo ni 12 kutoka Ukerewe, Sengerema (18), Ksimba (27), Magu (25), Ilemela (145), Misungwi (9), Buchosa (65) na Jiji la Mwanza (190).

Baadhi ya shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wanawake katka makundi ya lilyonufaika ni pamoja na Mama Lishe, ushoni, kuuza vifaa na bidhaa mbalimbali, kilimo na ufugaji wa kuku.

Katika ziara zake kutembelea vikundi vya ujasiriamali vinavyonufaika na mikopo hiyo, Mkuu wa mkoa wa Mwanza, John Mongella anasisisiza uwajibikaji na matumizi ya mikopo kwa malengo yaliyokusudiwa pamoja marejesho kuwa mionganoni mwa mambu muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa na wahuksika kufanya mikopo hiyo kuwa na tija endelevu.





MV Ukara II: Mtanzania kwa Watanzania

MWANDISHI WETU

MV Ukara II ni kivuko cha kihistoria katika Ziwa Victoria ambacho kinafanya safari zake kati ya Mwanza na visiwa vya Ukerewe. Ni cha kihistoria kwa sababu ya uamuvi wa serikali kuthamini kazi za wananchi wake ambaao kwa muda mrefu hawakuwa wakipewa nafasi katika kushiriki katika kazi kubwa nchini. Kwa serikali ya awamu ya tano, kivuko hiki ni zawadi ya Mtanzania kwa Watanzania.

Kivuko hicho kinetengenezwankampuniya Kitanzania, Songoro Marine yajijini Mwanza kwa thamani ya Shiling bilioni 4.2. Iwapo kivuko hiki kingetengenezwa nje ya Tanzania, kingeigharimu serikali Shiling bilion 32.

MV Ukara si tu kinalezea jinsi gani serikali ya awamu ya tano iliyowajali na kuishiriki sha sekta binafsi katika maendeleo ya Tanzania, bali pia ni kielelezo cha jinsi inavyowathamini wafanyabiashara

wazawa kwa kuwawezesha na kuwapa nafasi ya kufanya shughuli za maendeleo.

Ujenzi wa kivuko hiki ni sehemu ya jitihada za serikali katika kuhakikisha wananchi wake wanapata urahisi wa kusafiri kwa amani na usalama, hasa ikizingatiwa kwa muda mrefu usafiri katika maeneo ya vivuko umekuwa na shida. Ni sehemu ya ujenzi wa vivuko saba zikiwemo boti maalum ya wagonjwa (ambulance) tatu kwa ajili ya kusaidia usafiri katika mikoa mbalimbali hapa nchini veyne jumla ya thamani ya Sh. bilioni 36.3.

Wakati kivuko hicho kinazinduliwa rasmi katika Kisiba cha Ukara, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Elias Mwakalinga alisema kwamba ndani ya miakamitano serikali imejenga vivuko saba pamoja na ambulance maalum tatu.

“Baada ya ajali MV. Nyerere iliyozama Septemba 20, 2018 na kupoteza maisha

wananchi takribani 227, serikali iliamua kununua kivuko mbadala chenye urefu wa mita 42 na upana wa mita 10 na chumba maalumu cha kujifungulia hiyo ni kwa sababu serikali inawajali akinamama”

(Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Elias Mwakalinga)

ma”, alisema.

Alisema tatizo la usafirishaji na usafiri limetatuliwa na biashara zitafanyika kwa wingi zitakazo changia kukuza uchumi wa wananchi wa maeneo hayo na uchumi watanzania wote kwa ujumla.

“Kivuko hiki kinabeba

wananchi ambao serikali inawathamini sana kuanzia maisha yao pamoja na mali zao hivyo tusingependa masuala mengine kama yaliyotokea yatokee tunamuomba Mungu atuepushe”, aliongeza.

Akizungumzia katika uzinduzi huo, Waziri wa Ujenzi,

Uchukuzi na Mawasiliano kwa wakati huo, Mhandisi Isaack Kamwele aliezeza mkakati wa serikali kupambana na ajali zinazotokewa majini kwa kuwaagiza Shirkala la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kuhakikisha linaweka maofisa usimamizi katika maeneo yote ya usafiri majini, na kutoa mafunzo kwa wamiliki na waendeshaji wa vyombo vya majini ikiwamo Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania (TEMESA).

Alisema hatua hiyo itasidia kuongeza ufahamu juu ya umuhimu wa kuzingatia utaratibu na kanuni zinazosimamia uendeshaji wa vyombo hivyo kuepuka ajali.

Aidha, aliagiza TEMESA kusimamia kwa ukaribu uendeshaji wa vivuko hivyo ili wananchi wafaidi matunda mazuri ya serikali yao kwa furasa ya maendeleo yao binafsi.



MWANDISHI WETU

Miongozi mwa maeneo muhimu katika huduma ya maji ni ubora wa miundombinu ya majisafi na majitaka kuanzia kwenye vyanzo hadi kwa wananchi.

Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA, Leonard Msenyele kutoka na umuhimu wa miundombinu, shirika hilo la umma linatekeleza mradi wa maboresho unaogharimu euro14.6 milioni ambayo ni sawa na Sh 38.9 bilioni.

Mkataba wa utekelezaji wa mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya M/s. JOS. HANSEN & SOEHNE GmbH in JV with M/s. JR INTERNATIONAL BAU GmbH kutoka Ujeruman ulisainiwa Februari 16, 2017 kabla ya kazi kuanza rasmi Mei 26, 2017.

Mwauwasa na upanzu, uimarishaji huduma

Mhandisi Msenyele anafafanua kuwa kazi zinazotekelze na MWAUWASA ni uboreshaji na kupanua huduma ya majisafi katika maeneo ya milimani hususani maeneo yaliyo juu ya matenki ya maji ambayo haya-pati huduma kwa sasa ambayo ni Nyasaka, Bugarika, Nyengezi, Capripoint, Mjimwema, Nyakabungo na Kitangiri.

Anasema shughuli za mradi ambazo kwa sasa zinaendelea ni pamoja na ujenzi wa matenki ya maji katika maeneo ya Kitangiri (tenki moja la lita 500,000), Nyasaka (tenki moja la lita 1,000,000), Mjimwema (tenki moja la lita 1,200,000), Nyengezi (tenki moja la lita 1,200,000) na Bugarika (matenki mawili ya lita 700,000 na 250,000).

"Pia tunaendelea na kazi za utandazaji wa bomba za kusafirisha na kusambaza maji zenye vipenyo kati ya milimita 315 na milimita 50 jumla ya urefu bomba hizo ni mita 64,820," anasema na kuyataja maeneo yatakayonufaika na mradi huo kuwa ni Kitangiri, Kiseke, Nyasaka, Nyengezi, Bugarika, Mahina, Isamilo, Mjimwema/Nyakabungo na Nyankurunduma.

Kuhusu uboreshaji wa huduma ya majisafi kuititia ubadilisha wa mabomba ya zamani yaliyochakaa na kuongeza mtandao wa mabomba, anasema kazi hiyo inafanyika katika maeneo ya Makongoro, Nyakato na Barabara ya Kenya (Jumla ya urefu wa mabomba ni mita 15,770) na jumla ya mita 2,000 za mtandao wa mabomba zitaongezwa katika eneo la Makongoro.

Kazi nyingine kwa mujibu wake ni kubadilisha viungio katika mtandao wa majisafi - "Valves and Fire hydrants" kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kusambaza maji na kuongeza wigo wa kitengo cha Zimamoto kukabiliana na majanga ya moto najumla ya vifaa hivyo ni 22.

Anasema shughuli zingine zinazoendelea ni pamoja na kuboresha na kupanua mfumo wa majitaka kuititia utandazaji wa mabomba mapya na ubadil-



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan akikagua mradi mkubwa wa maji kwenye mji Nansio katika kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza mradi ambaa utahudumia wananchi 61,000.

Sh. bil 38.9 kuboreshaji miondombinu ya maji



isha wa mabomba ya zamani yaliyochakaa ambapo mabomba yenye jumla ya urefu wa mita 4,775 na vipenyo kati ya 600mm na 225mm yatatandazwa.

"Kazi hiyo inafanyika katika maeneo ya Mabatini "A" & "B", Kilimahewa, Isamilo, Igogo, barabaraya Kenyattana Makongoro. Pia kuongeza ufanisi wa mitambo ya kusukuma majitaka katika kituo cha Makongoro, Kirumba na Mwanza South," anasema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (kulia) wakimsikiliza, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga (kushoto) alipota maelezo kuhusu ujenzi wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Maji wa Misungwi katika kijiji cha Nyahiti Mkoani Mwanza.

Anasema mradi huo ambaa tekelezaji wake umefikia asilimia 90 ambapo hadi kufikia Machi 31 2019, utekelezaji wa Shughuli za Mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 75 na pindi utakapokamilika, mradi huo utanufaisha wakazi wapatao 105,649 waishio katika maeneo ya Jiji la Mwanza yaliyotajwa hapo juu na hiyo ni kwa tathimini ya mpaka kufikia mwaka 2028.

Huduma ya majisafi

Anasema utekelezaji wa mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Midogo ya Misungwi, Magu na Lamasi unatekelezwa kama sehemu ya Programu ya Kuboresha Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji hii Midogo (Misungwi, Magu na Lamadi).

Anasema shughuli za ujenzi wa mradi huo katika miji yote mitatu zinatetekelezwa na Kampuni ya M/s. CHINA CIVIL ENGINEERING CONSTRUCTION CORPORATION (CCECC) kutoka China kwa Mkataba mmoja wenyewe thamani ya euro 16,096,951.21 sawa na shilingi bilioni 42.657 ambazo ni gharama za jumla za mradi kwa Miji yote mitatu (3).

Anasema gharama za mradi huo kwa mji mdogo wa Misungwi ni euro 4,850,914.54 sawa na shilingi bilioni 12.855, Magu ni euro 6,404,169.56 sawa na shilingi bilioni 16.971 na Lamadi euro 4,841,867.11 sawa na shilingi bilioni 12.831.

Anasema mkataba wa utekelezaji wa shughuli za mradi ulisainiwa Februari 16,

2017 kati ya MWAUWASA na Mkandarasi, ambapo utekelezaji wa kazi za ujenzi wa mradi zilianza rasmi Mei 22 2017 kwa miji yote Mitatu na umekamilika kwa asilimia 85 na hadi kufikia Machi 31 2019, utekelezaji wa shughuli za mradi huo katika miji yote mitatu ulikuwa umekamilika kwa wastani wa asilimia 83.

Furaha ya wananchi

Mosi Richard mkazi wa Mabatini jijini Mwanza anashukuru serikali kwa kuwezesha ujenzi wa miundombinu maji ya kisasa katika eneo la Mabatini iliwayezeshwa kupatikana sasa huduma ya maji ya bomba kwa wananchi.

"Serikali imefanya kazi kubwa, sasa tumeyaona maji ingawa iboreshe maana kuna wakati yanakatika," anasema

Kwa upande wake Godfrey Maiko mkazi wa Nyakato anasema serikali ya awamu ya tano imejipambua kwa wananchi wanyonge, ambao kwasasakaribu maeneo mengi ya jiji la Mwanza wananchi wanapatu huduma za maji.

Kwa upande wake Godfrey Kiswene mkazi wa jijini Mwanza anasema maji katika jiji la Mwanza sasa ni raha tupu na kwamba ile kero ambayo wananchi walijukwa nayo imetoweka ingawa kwa baadhi ya maeneo machache huduma huwa maji yanakatika.

"Niombe Serikali yangu iendelee kuboresha huduma za maji ili maji yamiminike kwa wingi kwa wananchi," anasema.

Mapato, uchumi wyaimarika Mwanza



MWANDISHI WETU

Maendeleo ni mchakato mrefu unaogharimu muda, rasilimali fedha na utaalam.

Kote duniani maendeleo hupimwa katika misingi ya kuimarike na kuboreka kwa huduma za kijamii.

Ilikufikia maendeleo, ni lazima pawepo mikakati madhubuti na endelevu ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya muda mfupi, kati na mrefu.

Tangu ilivyoingia madarakanii Novemba 5, 2015, Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli imejipambanua kuwa na nia thabiti ya kujenga Tanzania mpya, Tanzania ya watu wanaochapakazi.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, Rais Magufuli amefanya mengi ya kupigwa mfano katika maendeleo ya sekta za afya, elimu, maji, usafirishaji, na miundombinu ya barabara.

Kazi zote zimefanyika kutekeleza ilani ya uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ahadi za Rais Magufuli wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2015 pamoja na ahadi au mahitaji mengine yanayotoka katika ziara mbalimbali za viongozi.

Kwa mkoa wa Mwanza, kazi nyingi na kubwa zimefanyika kuhakikisha upatikanaji wa maendeleo endelevu kwa wananchi.

Mkuu wa mkoa wa Mwanza, John Mongella anasema mikakati hiyo ya maendeleo inahusisha mazingira wezeshi kwa wananchi kufanya na kushiriki shughuli za uzalishaji mali kuanzia ngazi ya misingi hadi Taifa.

"Tunapozungumzia Tanzania yenye uchumi wa kati kuitia maendeleo ya sekta ya viwanda ifikapo 2015, tunalenga kumwezesha kila Mtanzania pale alipo kuzalisha, kuuza na kufanya biashara kulingana na mahitaji, mazingira na mtaji wake," anasema Mongella.

Sekta za kilimo, uvuvi, uwekezaji na biashara ni kati ya maeneo muhimu yanayotumiwa

Tunapozungumzia Tanzania yenye uchumi wa kati kuitia maendeleo ya sekta ya viwanda ifikapo 2015, tunalenga kumwezesha kila Mtanzania pale alipo kuzalisha, kuuza na kufanya biashara kulingana na mahitaji, mazingira na mtaji wake

(Mkuu wa Mkoa John Mongella)

na wakazi wa mkoa wa Mwanza kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Shughuli mbalimbali za kiuchumizinazotekelezwanawakazi wa mkoa huo umewezesha mkoa wa Mwanza kushuhudia ukuaji wa uchumi kwa kwa asilimia 8 huku pato la mkoa likiongezeka kila mwaka. Mongella anasema kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Taktamu, Pato la Mkoa wa Mwanza limeongezeka kutoka Sh10.05 trillioni mwaka 2016 hadi kufikia Sh11.3 trillioni mwaka 2017.

"Ongezeko la kipato inaimarisha uwemo wa wananchi wa kununua na kuuza; hii inatoa ishara njema kwa uchumi wa mkoa na mto mmoja mmoja," anasema Mongella

Makusanyo TRA

Mapato siyo tu yameongeze ka mifukoni mwa wananchi wa kawaada, bali hata Mamla-ka ya Mapato mkoani Mwanza pia imeongeza makusanyo ya kodi na ushuru mbalimbali



za Serikali. Ongezeko hilo lime-shuhudiwa kati Julai 2018 hadi Juni 2019 ambapo mapato TRA mkoa wa Mwanza imokusanya zaidi ya SH173,456,148,241.79i kilinganishwa na shilingi 157.1 bilioni kulinganisha na Sh142.6 bilioni zilizokusanya kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Juni 2018. Ongezeko hilo ni zaidi ya Sh16.3 bilioni, sawa na asili-

mia 10.3. Kwa mujibu wa mkuu wa mkoa, hata makusanyo katika halmasauri nane za mkoa huo pia yaliongezeka kati Julai 2018 hadi Juni 2019.

Ili kujiongezea mapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, halmasauri zamkoawa Mwanza zimeanzisha nakutekeleza miradi ya kimkakati ambapo kwa Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela miradi hiyo inahusisha ujenzi na ukarabati w a miundombinu katika masoko, vituo vya mabasi na maegesho ya magari.

Mbali na viwanda na sekta ya madini, shughuli nyingine za kiuchumi jijini Mwanza ni pamoja na kilimo na uvuvi

